JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# UKUAJI WA UCHUMI VIJIJINI NA UPUNGUZAJI WA UMASKINI TANZANIA

Imetolewa na Kikundi cha Kitaalamu cha Utafiti na Uchambuzi cha Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA

MUHTASARI 3 RIPOTI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA BINADAMU YA MWAKA 2005

**Upunguzaji wa umaskini wenye maana nchini Tanzania utategemea ukuaji uchumi wa viwango vikubwa katika maeneo ya vijijini, hususan katika sekta ya kilimo. Huu ni muhtasari wa vikwazo vya maendeleo vinavyokabiliwa na wazalishaji wadogo na mwelekeo mpana wa uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara. Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2005 (PHDR) inapendekeza kwamba upangaji wa mipango unganifu ya uzalishaji ifikiriwe kama mkakati wenye kuweza kuleta mafanikio ya kupambana na vikwazo. Hii inahusisha upatikanaji ulioratibiwa wa pembejeo zilizoboreshwa, huduma za ugani, usafirishaji, usindikaji na masoko. Ripoti hii pia inasisitiza jukumu muhimu ambalo vyama vya wazalishaji vitakuwa nalo katika kuendeleza na kulinda matakwa ya wakulima wadogo katika mifumo unganifu kama hii.**

## Hali ya Sasa ya Kilimo cha Wakulima Wadogo


Sampuli ya Sensa ya Kilimo ya Taifa (2002/03) inakadiria kwamba nchini Tanzania wapo wakulima wadogo wapatao milioni 4.8 wanaolima takriban hektari milioni 44. Kilimo kwa kawaida ni kile kinachotumia nguvu kazi ya familia na uzalishaji hautoi mazao mengi; ni kwa ajili ya kujikimu zaidi. Kaya za wakulima wadogo kwa kawaida huwa na wakazi vijana walio na umri chini ya miaka 20 (53%). Asilimia 31 ya wakuu wa kaya hawana elimu, wakati asilimia 63 wana kiwango fulani cha elimu, ijapokuwa ni asilimia 20 tu kati yao wamemaliza darasa la nne.

Kuhusu matokeo ya uzalishaji, wengi wa wakulima wadogo hutegemea zao moja tu kama chanzo cha mapato. Uzalishaji wa mazao ni shughuli kuu kwa karibu asilimia 50 ya kaya za wakulima wadogo. Karibia asilimia 70 ya wakulima wadogo wana chanzo kimoja au zaidi cha mapato nje ya kilimo. Kaya nyingi zinazozalisha mazao hutumia kile wanachozalisha, wakati asilimia 70 huuza sehemu fulani ya mazao yao. Kuna viwango vidogo sana vya usindikaji na uhifadhi wa mazao nje ya ngazi ya kaya. Upatikanaji wa masoko ni changamoto kwa wale wachache wanaosema kwamba vikwazo vya kitaasisi vinahusiana na bodi za kisheria za kiserikali, jumuiya za wafanyakazi, vyama vya wakulima na vyama vya ushirika.

Kuhusu pembejeo kwa ajili ya uzalishaji, asilimia 63 ya kaya zilisema kwamba zinatumia ardhi yote walio nayo. Kwa jumla, upatikanaji wa ardhi unatofautiana sana kati ya mkoa na mkoa. Kaya nyingi za wakulima wadogo hulima kwa kutumia jembe la mkono – chini ya kaya 40,000 za wakulima wadogo zinamiliki trekta, na trekta hizi hutumika na takriban kaya 140,000 za wakulima wadogo kwa jumla. Umwagiliaji hutumika mara chache sana (8%) na wakulima wadogo, na ni hekta kama 125,000 tu zinazomwagiliwa.


Asilimia 26 ya wakulima wadogo hutumia mbolea kwa ajili ya kuboresha udongo na chini ya asilimia 20 hutumia aina mojawapo ya pembejeo (ikiwemo mbolea iliyotokana na mchanganyiko wa vitu). Pembejeo za kisasa kama vile samadi, madawa ya kuua wadudu na mbegu bora hutumika kwa nadra. Utumiaji wa samadi unabaki mdogo katika maeneo mengi ya nchi; isipokuwa katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, na Kilimanjaro, ambapo karibu asilimia 30 ya kaya zimeripotiwa kutumia samadi. Mikoa mitatu ya kwanza kati ya hii ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wanne wa mahindi nchini.

Asilimia 3 tu ya kaya hutumia mikopo kugharamia shughuli za kilimo. Kati ya kaya hizo zinazochukua mikopo, karibu theluthi moja huchukua mikopo kutoka katika vyama vya ushirika na theluthi nyingine kutoka kwa wanafamilia, marafiki au ndugu. Uchukuaji huu wa mikopo ni kwa ajili ya samadi, madawa ya kilimo na mbegu; mikopo michache huchukuliwa kwa ajil ya zana, nguvu-kazi na umwagiliaji. Kaya chache zinaweza kuweka akiba ili kununulia bidhaa za thamani au




**KIELELEZO 1: MIELEKEO KATIKA UZALISHAJI WA MAZAO YA BIASHARA, 1995-2004**

Chanzo: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tafiti za Kiuchumi, miaka kadhaa




**KIELELEZO 2: MIELEKEO YA UZALISHAJI YA MAZAO MAKUU YA CHAKULA, 1995-2004**

Chanzo: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tafiti za Kiuchumi, miaka kadhaa

tekinolojia mpya za uzalishaji.

Kama asilimia 35 tu za wakulima wadogo walipata ushauri wa wahudumu wa ugani katika mwaka 2002-03, lakini kulikuwa na tofauti kubwa kimkoa. Ushauri mkubwa (asilimia 93) ulitoka serikalini.

## Mielekeo ya Uzalishaji

Uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara kwa jumla yamekuwa yakibadilikabadilika katika viwango vya chini katika miaka kumi iliyopita, huku uzalishaji wa baadhi ya mazao ukiwa unashuka. Matokeo haya yanatokana na wazalishaji wadogo na wakubwa.

Kwa muhtasari, uzalishaji wa chai, tumbaku, katani na kahawa umeenda ukibadilikabadilika kwa kiwango cha kama tani milioni 50 kwa mwaka; wakati mpunga, maharage, mtama na uwele vimekuwa vikibadilika kwa kiwango cha tani nusu milioni kwa mwaka. Mahindi na mihogo imekuwa ikiongezeka tangu mwaka 2002. Wakati huo huo uzalishaji wa pamba, korosho na miwa umeonesha ongezeko kubwa sana, uzalishaji wa miwa ukiongozeka kwa kiwango kikubwa kuanzia mwaka 2001. Hii inatokana na ubinafsishaji wa mashamba ya miwa na utumiaji wa mfumo wa 'out-grower' wa uzalishaji, ulioanza mwanzoni mwa mwaka 2000.

Kuboresha ubora wa viwango vya mazao ya kuuza nje kutoka Tanzania pia hutoa changamoto. Inafurahisha kuona kwamba kahawa ya Tanzania na Kenya ilipata bei sawa ya wastani kabla ya mwaka 2000, lakini baada ya muda bei ya kahawa ya Tanzania ilishuka chini zaidi ya kahawa kutoka Kenya. Mavuno ya chai kutoka kwa wakulima wadogo yamekuwa yakiendelea kuwa madogo kuliko mavuno kutoka katika mashamba makubwa kuanzia katikati ya miaka ya 1970 hadi 2005; huku tija ya mashamba makubwa ya chai ikiongezeka katika miaka ya kati hadi ya mwishoni mwa mwaka 1990 wakati ule wa wakulima wadogo ukishuka kwa kiwango kikubwa sana. Hali ilikuwa hivi hivi kwa mazao mengine, ambapo uzalishaji wa mahindi na wakulima wadogo (mwaka 2002/03) ulikuwa tani 0.73 kwa hekta na ule wa uwele ukiwa tani 0.43 kwa hekta ambao hauwezi kulinganishwa na uzalishaji wa wakulima wakubwa wa tani 4.0 kwa hekta wa mahindi na tani 2.7 kwa hekta wa uwele.

## Kuongeza Ukuaji wa Uchumi katika Maeneo ya Vijijini

Mfumo wa kilimo uliopo hivi sasa kwa kiwango kikubwa ni wa mtu mmoja mmoja, usioratibiwa na usio na ufanisi, wenye viwango vidogo vya uwekezaji. Kinachohitajika ni mfumo unganifu, wenye ufanisi, wenye mwitikio na wenye kushikamana. Wakulima wadogo wanahitaji msaada wa kuongeza tija, ubora, na uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazotokana na masoko ya ndani na nje. Lengo ni kugeuza sekta ya kilimo iwe sekta yenye tija kubwa na mazao yenye viwango vya juu. Hii inahitaji kufikiria upya mkabala unaotumika kwenye uzalishaji wa kilimo – hasa kwa wakulima wadogo.

## Mifumo Unganifu ya Uzalishaji

Mifumo unganifu ya uzalishaji inaweza kuwa njia mojawapo ya namna ya kuendelea kwa baadhi ya maeneo. Inajulikana kwa ajili ya mkabala wa kiuratibu wa pembejeo zilizoboreshwa, huduma za ugani, usafirishaji na masoko. Inajenga uwezo wa wakulima kwa njia ya kutoa huduma za ugani na ufuatialiaji wa karibu wa uzalishaji na ubora.

Mifumo unganifu ya uzalishaji imekuwa ikipanuka kwa

karibu miaka mitano hivi nchini Tanzania, zaidi kama mifumo ya 'out-grower'. Matokeo yake ni maeneo yaliyopanuka ya kulima, ongezeko la uzalishaji na tija, na ongezeko la ubora. Kwa mfano, Rungwe, uzalishaji wa majani ya kijani ya chai kwa mwaka umeongezeka mara tano zaidi katika miaka minne iliyopita – kutoka kilo 3,774,912 kwa hekta mwaka 2000/01 hadi kilo 15,285,451 kwa hekta katika mwaka 2004/05. Mavuno ya wastani ya majani ya kijani kutoka kwa wakulima wadogo waliounganishwa kwenye mfumo pia yamekuwa yakiongezeka kwa kufuatana kutoka kilo kama 1,000 kwa hekta mwaka 2000 hadi kilo kama 5,000 kwa hekta mnamo mwaka 2004, wakati ubora wa jumla wa chai kutoka kwa wakulima wadogo imeripotiwa kuzidi kipeo kilichowekwa na kampuni inayowaendeleza, Kampuni ya Chai ya Wananchi.

Mifumo unganifu ya uzalishaji inatofautiana katika mambo fulani lakini kipimo cha msingi kinahusisha mfumo wa uratibu wa karibu wa uzalishaji, huduma za ugani, usafirishaji, usindikaji na masoko. Mifumo hii kwa kawaida inahusisha misaada ya kitaalamu kutoka katika makampuni ya nje au ya ndani ya nchi. Mifumo hii na ina vituo vya ukusanyaji taarifa kwa wakulima, wasindikaji na masoko. Inawapa wakulima vivutio na misaada ya kiushauri ili kuongeza uzalishaji na ubora.

Sifa kuu za Mifumo Unganifu ya Uzalishaji ya Kitanzania imetolewa kwa muhtasari hapa chini kwa kutumia mifano ya Kampuni ya Chai ya Wananchi (WATCO), Katani Ltd (Katani) na Kiwanda cha Sukari cha Kilombero:

- Shughuli zote kuanzia uzalishaji mpaka masoko ni vipengele vya kila kimojawapo cha mifumo hii. Hii ni muhimu kwa ajili ya udhibiti wa wingi na ubora, na kwa ajili ya mawasiliano kati ya kampuni na wakulima wadogo. Shughuli hizi zinajumuisha: uzalishaji, huduma za ugani, usafirishaji, usindikaji na masoko.

- Miundo ya kiuendeshaji inatofautiana. Wakulima wanaweza wakawa wote, au wachache. Wengi ni wakulima wadogo wenye kuhusishwa kidogo katika kampuni inayowaendeleza. Au, wakawa na hisa katika kampuni na/au wenye wawakilishi kwenye bodi ya wakurugenzi ya kampuni zinazowaendeleza.

- Utumiaji wa mawakala hutokea, mara nyingi zaidi kwenye huduma za ugani na usafirishaji, kuliko kwenye maeneo ya usindikaji na masoko. Hii inatoa fursa za kuunda ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

- Uzuiaji wa haki za matumizi ya ardhi za wakulima wadogo ni kipengele muhimu sana kwa kila kimojawapo cha mifumo hii.

Mifumo unganifu yenye ufanisi hutoa motisha na tuzo kwa wadau wote, kwa sababu inategemeana na upatikanaji wa matokeo yenye faida. Thamani iliyoongezeka kwenye mlolongo wa bidhaa inatakiwa iwape faida wale wote wanaohusika, ingawa uimara wa kiungo kati ya wadau utategemea ukubwa, uwezo na mifumo ya kiuendeshaji ya wakulima wadogo na wa kampuni inayowaendeleza. Hii ni tofauti na michakato ya uzalishaji ambayo siyo unganifu, na pale ambapo motisha kwa wakulima wanaojitegemea iko nje ya mfumo wa uzalishaji – usindikaji – masoko kwa jumla. Vilevile, uzalishaji huongezeka na kuboreshwa bila kuathiri haki za wakulima wadogo kwa namna hasi, umiliki wao wa ardhi, au kuwageuza kuwa vibarua.

## Changamoto Zinazokabili Mifumo Unganifu ya Uzalishaji

Mifumo unganifu ya uzalishaji ipo katika mazao mbalimbali na inaweza kuwa na umuhimu kwa sekta kama vile uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na maziwa. Hata hivyo, zipo changamoto nyingi. Wazalishaji wanaweza kuuza bidhaa zao kwa wanunuzi walioko nje ya mfumo kwasababu wanaweza kupata bei nzuri zaidi kwa 'wanunuzi huru' (wale ambao hawana uhusiano na kampuni na ambao hawajawekeza katika mifumo ya uzalishaji iliyoboreshwa). Kivutio kingine ni kwamba kwa kumwuzia mtu baki, mkulima anaweza kuepuka ulipaji wa fedha zilizokopwa kutoka kwenye mfumo. Ufumbuzi wa tatizo hili unaweza kuhusisha mikataba ya kisheria – ingawa hii inaweza kuwa migumu kushurutisha, na ridhaa inayotokana na faida kubwa zaidi ya kubaki ndani ya mfumo inahitajika.

Changamoto nyingine ni kwamba mfumo unaweza kuwa wa ukiritimba na kampuni inayoendeleza kutoza fedha zaidi kwa ajili ya pembejeo au kutoa bei za chini kwa mazao. Ufumbuzi wa tatizo hili utategemeana na nguvu tofauti za wahusika mbalimbali, mchango wa uzalishaji wa wakulima wadogo kwa kampuni yote na kiwango walichojiandaa. Sheria na kanuni imara zaidi vinaweza pia kusaidia kulinda matakwa ya wakulima wadogo.

## Vyama vya Wazalishaji

Vyama vya uzalishaji vilivyo imara vinahitajika katika mipango unganifu ili kuhakikisha kuwepo kwa haki za kazi za wakulima wadogo, umiliki wa ardhi na magawio sawa katika faida za ongezeko katika uzalishaji. Vyama vya ushirika ndio aina inayotawala ya vyama vya

wazalishaji nchini Tanzania ingawaje kwa kiwango kinachoongezeka, mifumo mingine ya kisheria inaundwa. Vyama vinaweza kuwezesha upatikanaji wa mahitaji kama vile tekinolojia na mikopo, na kupunguza gharama kupitia viungo vya mlolongo wa ugavi na ushindani.

Vyama vya ushirika vinaweza kuwa na faida panapokuwa na ushirikishwaji wa dhati wa wanachama. Kupitia vyama vya ushirika, wakulima wadogo wanaweza kuendeleza upatikanaji wa mahitaji yao, masoko, kuhakikisha viwango vya bidhaa na kupata taarifa, huduma za ugani na mikopo. Vyama vya ushirika vinaweza kuunganishwa na vingine vilivyo juu ili kuviruhusu viendeshwe kama sehemu ya mipango uganifu ya uzalishaji.

Shinikizo la vyama vya ushirika lilikuwa kubwa katika miaka ya 60 nchini Tanzania na majaribio ya hivi karibuni ya kuliibua upya yanaweza kuchukuliwa kama hatua katika mwelekeo sahihi. Mageuzi yanafanyika katika mazingira ambayo, katika maeneo mbalimbali nchini kiwango cha kitaasisi kwa ajili ya vyama vya kidemokrasia vya ushirika kimeporomoka, shinikizo la vyama vya ushirika limepoteza uhalali kutoka kwa wanachama wake, wako walio dhaifu kifedha na hawako tayari kwa mashindano ya kiulimwengu.

Hii inatoa changamoto kuu tatu kwa mtindo wa vyama vya ushirika kufanikiwa: kwanza, ni lazima iwe chaguo lenye uwezo wa kumea na lenye manufaa kwa wakulima wadogo, na ni lazima imani ya wakulima hao kuhusu mtindo wa vyama vya ushirika irudishwe. Pili, vyama vya ushirika ni lazima vihakikishe uunganifu wa uzalishaji, usafirishaji, usindikaji na masoko ili viweze kutumia vizuri ongezeko la thamani la mfumo wa ugavi na mahitaji. Mwisho, vyama vya ushirika ni lazima viendelee kutoa maarifa na uvumbuzi kwa namna ambayo thamani yake inalingana na gharama na kuhakikisha kwamba taarifa hizi zinawafikia wanachama kwa namna ambayo ni rahisi kupatikana na kueleweka.

## Hitimisho

Kwa jumla, viwango vya sasa vya uzalishaji wa kilimo havitoshi kufikia shabaha za MKUKUTA. Upunguzaji wenye maana wa umaskini utategemea sekta ya kilimo kufanikisha kiwango cha ukuaji endelevu cha asilimia 6 kwa mwaka. Ukuaji huu ni lazima uwe wenye msingi mpana, na mikakati ya kufanikisha hili ni lazima iandaliwe na kutekelezwa.

Ukuzaji wa mipango unganifu ya uzalishaji inayohusisha upatikanaji wa mahitaji, tekinolojia na huduma za ugani, usafirishaji, usindikaji na masoko vinaweza kuongeza ukuaji wa uchumi vijijini. Vipengele hivi ni lazima vipatikane kwa wakati unaotakiwa, na havina budi, vipatikane kwa urahisi, na viwe vinavyofaa kwa bidhaa na mzalishaji. Hii itahakikisha ongezeko la uzalishaji na uboreshaji wa kiwango cha bidhaa.

Jukumu la Serikali katika kuhakikisha kuwepo kwa mazingira kwa ajili ya ukuzaji na uendeshaji wa mipango unganifu ya uzalishaji kama hii, ukiwemo utoaji wa msaada kwa ajili ya ukuzaji wa miungano ya wazalishaji ni muhimu sana.

Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2005 inatoa taarifa muhimu kuhusu viwango na mwelekeo wa umaskini nchini Tanzania, ikilinganisha na malengo kutoka katika Malengo ya Milenia ya Maendeleo, Mkakati wa Kutokomeza Umaskini (MKU) na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Ripoti hii inapatikana katika nakala pepe, na ripoti iliyochapishwa inaweza kupatika kutoka:

**Kitengo cha Kuondoa Umaskini, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Dar es Salaam.**

Simu: (022) 2113856 / 2124107

Barua pepe: mkukutamonitoring@gmail.com

Anwani ya tovuti: http://www.tanzania.go.tz/poverty/index.html/

na kutoka **REPOA (Utafiti kuhusu Utokomezaji wa Umaskini)**

Simu: (022) 2700083

Barua pepe: repoa@repoa.or.tz

Anwani ya tovuti: http://www.repoa.or.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA